Maana ya Ibada.

مفهوم العبادة.

< السواحلية – سواحيلي – Swahili >

Shaykh Muhammad ibn Saalih al-'Uthaymeen
(Allah amrehemu)
سماحة الشيخ محمد بن صالح بن عثيمين (رحمه الله)

Imetafsiriwa na: Kitengo cha Lugha ya kiswahili, katika Tovuti ya IslamHouse.com

Imepitiwa na: Yunus Kanuni Ngenda.

ترجمة : فريق القسم السواحلي بموقع إسلام هاوس

مراجعة: يونس كنون نغندا

Maana ya Ibada.

SWALI:

Nini maana ya Ibada? Je, ina maana ya ujumla na maana maalumu?.

JAWABU: Ibaada ina maana mbili:

A.Maana ya ujumla.

B.Maana maalumu.

Maana yake kwa ujumla nikama tulivyo eleza katika swali la kwanza ya kwamba: ni kudhalilika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kupenda na kutukuza kwa kufanya amri zake na kujiepusha na makatazo yake katika njia iliyo elekezwa na sheria zake.

Hii ndio maana yake kwa ujumla.

Maana yake maalum - nakusudia kwa urefu- Amesema Sheikhul-Islam Ibnu Taimiyya (r.h): Ni jina lililo kusanya kila anacho kipenda Mwenyezi Mungu na kukiridhia kutokana na maneno na vitendo vya siri na dhahiri,

Mfano: Khofu, Unyenyekevu, Kutegemea, Swala, Zaka, Funga, na ibada nyinginezo tofauti na hizo zilizopo katika sheria ya Uislamu.

Na ukiwa unakusudia maana ya ibada kwa ujumla au kwa maana maalum kama walivyo taja badhi ya wanachuoni ya kwamba Ibada yawezekana ikawa ya kidunia au ya kisheria.

Kwa maana ya kwamba yawezekana binadamu akadhalilika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini ikawa kwa sababu ya dunia, na yawezekana ikawa kudhalilika kwa sababu ya kisheria.

Ibada za kidunia ni kwawote, Muislamu, Kafiri, Mwema, Muovu. Kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Hapana yeyote aliomo

mbinguni na ardhini ila atafika kwa Arrahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa wake). (Maryam: 93).

Vyote vilivyopo mbinguni na duniani ni vyenye kunyenyekea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa yale aliyo ya panga, haiwezekana kiumbe akaenda kinyume na matakwa ya Allah katika mambo aliyo ya kadiria.

Lakini Ibada maalum nazo ni ibada za kisheria ni kudhalilika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kisheria, ibada hizi ni maalumu kwa waumini wenye kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, wenye kusimama katika amri zake.

Kisha miongoni mwa ibada kuna ibada maalum zaidi. Zile ibada maalumu nizile za Mitume (s.a.w), mfano kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake). (Al-Furqan: 1).

Na kauli yake: (Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu). (Al-Baqara: 23.)

Na kauli yake: (Na wakumbuke waja wetu, Ibrahim na Is-haqa na Yaa'qubu). (Swad: 45.)

Na dalili nyingine tofauti na hizo zinazo wasifia Mitume (s.a.w), kuonyesha kama na wao ni waja wake.

Je, wanalipwa thawabu wale wanao dai kufanya ibada kwa kuamini matendo ya Mwenyezi Mungu kama kuumba na kufisha na kuhuyisha, bila kufanya ibada alizo zifaradhisha Mwenyezi Mungu kama kutoa shahada na kuswali na kufunga …nk. ?

JAWABU: Hao hawalipwi, kwasababu wanadamu wote wameubwa na Mwenyezi Mungu wakiwa katika maumbile ya kukiri ukubwa wa Mwenyezi Mungu na vitendo vyake katika ulimwengu na hilo nilazima kwa watu wote, mwanadamu anauguwa na anakuwa masikini, na anampoteza kipenzi chake bila yeye kupenda, bali halipendi jambo hilo, lakini ni lazima iwe hivyo kwa sababu nimatashi ya Mwenyezi Mungu.